# NYUMBA

## MSAMIATI WA NYUMBA

- Nyumba
- Vifaa vya nyumbani
- Familia
- Nyumbani
- Safisha
- Sehemu za nyumba
- Vitu katika nyumba

## SEHEMU ZA NYUMBA

- Chumba cha kulala (bedroom)- mahali watu hulala
- Sebule (sitting room)- mahali ndani ya nyumba ambamo watu huzungumzia au kupokelea wageni
- Chumba cha maakuli (dining room)- chumba ambamo watu wanakaa na kula chakula
- Bafu (bath room)- chumba cha kuogea
- Paa (roof)- sehemu ya juu ya nyumba
- Mlango (door)- mahali pa kuingia nyumbani au chumbani
- Dirisha (window)- sehemu ndogo kwenye ukuta inayoleta mwanga na hewa safi
- Ukuta (wall)- sehemu ya nyumba inayotofautisha vyumba mbalimbali
- Nguzo (pillar)- sehemu ya nyumba ambayo inashikilia uzito wa nyumba
- Baraza (veranda)- sehemu nje ya nyumba iliyo na paa
- Ua (compound)- sehemu nje ya nyumba
- Ufinga (outside resting place)- sehemu nje ya nyumba ya kukaa na kupumzika
- Shuli (back yard) – sehemu ya nyuma ya nyumba
- Sakafu- sehemu ya chini ya nyumba
- Korido /ushoroba (corridor)- sehemu nyembamba ndani ya nyumba baina ya vyumba
- Dari (ceiling)- sehemu inayofuka kikomo cha juu cha nyumba
- Jikoni (kitchen)- mahali vyakula hupikiwa
- Stoo (store)- mahali vitu vya nyumbani huhifadhiwa
- Choo (toilet)– mahali pa kwenda haja kubwa au ndogo

## VITU VINAVYOPATIKANA KATIKA SEHEMU MBALIMBALI ZA NYUMBA

### JIKONI

- Sufuria
- Mwiko
- Sahani
- Kijiko
- Uma
- Jiko la makaa
- Jiko la umeme
- Jiko la gesi
- Kabati
- Rafu
- Jokofu/ friji/ jirafu n.k

SEBULENI

- Makochi
- Viti
- Meza
- Televisheni / Runinga
- Redio/ Mwengoya
- Pazia
- Zulia
- Mkeka n.k

BAFU NA CHOO

- Sabuni
- Msuguo
- Taulo
- Maji
- Karatasi ya shashi
- Beseni n.k

CHUMBA CHA KULALA

- kitanda
- blanketi
- shuka
- chandalua
- kabati/ sanduku la nguo
- patipati n,k

STOO

- vyakula mbalimbali
- vifaa vya kutumia shambani kama jembe, panga , shoka n.k
- vikapu

ZOEZI

A. Kwa kutumia maneno yaliyo kwenye boksi kutegua vitendawili vifuatavyo; mimi ni nani?

| |
|---|
| Dari, sebule,jikoni, stoo, baraza, dirisha, paa, bafu, choo, mlango, chumba cha kulala, chumba cha maakuli. |

i. Mimi ni mahali pa kwenda haja. Mimi ni nani?
ii. Mimi ni chumba cha kuogea. Mimi ni nani?
iii. Mimi ni ukumbi ndani ya nyumba wa kuzungumzia au kupokelea wageni. Mimi ni nani?
iv. Mimi ni sehemu ya nyumba ambamo watu hulala. Mimi ni nani?
v. Mimi ni chumba maalumu ambamo chakula hupikiwa. Mimi ni nani?
vi. Mimi ni chumba maalumu ambamo watu wanakaa kula chakula. Mimi ni nani?
vii. Mimi ni sehemu ya nje ya nyumba ambayo watu hukaa kwa ajili ya mazungumzo. Mimi ni nani?
viii. Mimi ni sehemu ya juu ya nyumba iliyoezekwa kwa mabati au nyasi au magugu au mafujo. Mimi ni nani?

B. Tumia maneno sahihi kutokana na boksi ili kukamilisha sentensi zifuatazo.

| |
|---|
| Kijiko, sahani, taa, ufagio,kisu, sufuria, sabuni, kiti, jembe, kitanda, uma, mswaki |

i. Ninaomba kutumia …………………… kupata mwangaza wa kutosha.
ii. Ninataka kutumia ……………….. kunywa mchuzi kutoka kwenye sahani.
iii. Tumia ………………….. kunawa mikono baada ya kutoka msalani.
iv. Mama anatumia ………………… kufagia jikoni.
v. Kato anatumia ……………… kulima shambani.
vi. Dada yangu anapiga …………….. meno yake.
vii. Msichana analala ……………………………
viii. Mama anapika viazi katika ……………………..

C. Soma habari ifutayo kisha ujibu maswali.

Jina langu ni Nakato Aisha. Ninasoma kidato cha kwanza katika shule ya sekondari ya wasichana ya Moroto. Ninasomea Moroto lakini nyumbani kwetu, ninatoka katika kijiji cha Idudi wilayani Iganga. Kila likizo, ninafurahia kukaa nyumbani na watu wa familia yangu. Nyumba yetu ni kubwa na tena nzuri sana. Baba na mama wanatwambia kila siku kutunza vizuri vitu katika nyumba yetu. Kwa mfano, wanatuambia, tusicheze kwa kurukaruka kwenye viti na makochi.

Viti na makochi tunavikalia sebuleni. Wakati mwingi tunakaa kwenye makochi tukitazama televisheni. Tunapenda kutazama vipindi mbalimbali kama vile taarifa ya habari, michezo ya kuigiza, vibonzo na mambo mengine ya kufurahisha.

Kazi ninayopenda kufanya nyumbani ni kusafisha vyombo vya jikoni. Vyombo vya jikoni vinatumika katika kazi mbalimbali. Kwa mfano tunakula chakula kwa kijiko na uma. Tunamenya ndizi na kukata nyama kwa kisu. Tunatumia sahani kula chakula. Ukitaka kunywa uji, unatumia kikombe. Halafu, tunatumia sufuria kupika chakula. Ninapenda kusaidia wazazi wangu katika kutunza vitu vya nyumbani kwa sababu ni vitu vyetu sote kama familia.

Maswali

i. Pendekeza kichwa cha masimulizi haya mliyosoma. (suggest a suitable title for this story you have read)
ii. Msimulizi anaitwa nani na anasomea wapi? (what is the name of the narrator and where does she study from)
iii. Andika kijiji cha msimulizi anakoishi na familia yake. (write the village that the narrator stays with her family members )
iv. Kwa nini si vizuri watoto kucheza kwa kurukaruka kwenye viti na makochi? (why is it not good for children to play and jump on the chairs and sofa sets?)
v. Taja umuhimu wa televisheni nyumbani? (mention the importance of a television at home)
vi. Msimulizi anapenda kufanya kazi gani nyumbani? (what type of work does the narrator like doing at home?)
vii. Msimulizi anataka kumenya ndizi. Atatumia nini? (the narrator wants to peel bananas. What will she use?)
viii. Andika sentensi tatu zinazohusu namna unavyotunza vitu vya nyumbani kwenu. (write three sentences about how you take care of items at your home )

NGELI YA U-ZI